“Hakika Mbingu Itakuwa Bora Kuliko Vyote”

(“Heaven Will Surely Be Worth It All”)

Na

Ellis P. Forsman

“Hakika Mbingu Itakuwa Bora Kuliko Vyote”

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

“Hakika Mbingu Itakuwa Bora Kuliko Vyote”

Rum. 8:14-25

Kuna wapi unaoitwa, “Hakika Mbingu Itakuwa Bora Kuliko Vyote”. Maneno haya yameandikwa na W. Oliver Cooper na mashairi yamepangwa na Minzo C. Jones.

Ninapouimba wimbo huu, mawazo mawili makuu huja katika akili yangu:

- Dhabihu nyingi ambazo Mkristo mwaminifu anapaswa kutoa mara nyingi.
- Utukufu wa mbinguni na kitakachokuja kwa wale watakaobaki kuwa waaminifu.

Wimbo unasema kwamba thawabu zitakuwa bora kwa gharama yoyote; kama alivyosema Paulo, akiwaandikia Warumi. Rum. 8:18, “*Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu*.”

Na tena, katika kuwaandikia Wakorintho. 2 Kor. 4:17, “*Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi;*”

Je mbingu itakuwa bora kuliko vyote? Ndiyo! Lakini haiumizi kukumbushwa gharama na zawadi ya uanafunzi.

Gharama ya uanafunzi

Ni lazima Yesu awe wa kawanza katika maisha yetu.

Kabla ya mtu binafsi. Luka 9:23-24, “*Akawaambia wote, mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku anifuate. Kwa kuwa mtu atakaaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha*.”

Kabla ya mtu yeyote, pamoja na familia.

- Luka. 14: 26, “*Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na make wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.*”
- Mat. 10:34-37, “*Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani bali upanga, kwa maana nalikuja kumfitini mtu na babaye, na binti na mamaye, na mkwe na mkwe mtu; na adui za mtu ni wale wa nyumbani mwake. Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili.*”

Kabla ya chochote ambacho ulimwengu unapaswa kutoa.

- Luka 9:25, "*Kwa kuwa namfaa nini mtu kuupata ulimwengu wote, kama akijiangamiza au kujipoteza mwenyewe?*"
- Luka 14:33, "*Kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.*"

Lazima tukubali kuteseka kwa ajili ya Kristo.

Lazimaa tukubali kubeba msalaba weetu wenyewe. Luka 14:27, "*Mtu yeyote asiyeuchukua msalaba wake na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.*"

Kuishi katika ulimwengu usio wa uungu, tunaweza kupata kwamba kumfuata Kristo wakati mwingine hujumuisha dhihaka na mateso. 2 Tim. 3:12, "*Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa.*"

Mateso yanaweza kuwa ya kimwili. 1 Pet. 4:12-13, "*Wapenzi msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. Laakini kama mnaavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe.*"

Mateso yanaweza kuwa yam domo. Luka 6: 27-28, "*Lakini nawaambia ninyi mnaosikia, wapendeni adui zenu, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi, wabarikieni wale ambao wawalaani ninyi, waombeeni wale ambao wawaonea ninyi.*"

Vitu vingine ambavyo tunapaswa kuvumilia kwa ajili ya Kristo:

Udhaifu binafsi katika jitihada zetu dhidi ya dhambi. 1 Kor. 9:27, "*Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.*"

Kukatishwa tama kunakotokana na ndugu walioshindwa. 2 Kor. 11:29, "*Ni nani aliyedhaifu, nisiwe dhaifu nami? Ni nani aliyekwazwa name nisichukiwe?*"

- Wale ambao kutojali kwao na kukataa huzaa huduma yenye wivu.
- Wale ambao maudhrio yao ya kila mara husababisha ugumu wa kuwategemea.
- Wale ambao kutopenda kwao kuhudumu utengeneza mzigo wa ziada kwa wale wanaohudumu.
- Wale ambao manung'uniko yao huzuia juhudi ya hao wanaojaribu kufanya kitu.

Hatakama tumejaliwa kuyakimbia vitu hivyo, lazima tuwe tayari kutumia muda wetu na jitihada katika kufanya kazi ya Kristo.

- Wakati mwingine pekee yetu, au na wachache wa kutusaidia.
- Wakati mwingine kaatika sehemu ngumu, ambapo wachache hushukuru juhudi zako.

Ndiyo, uanafunzi unaweza kugharimu.

Kama wimbo unavyopendekeza, maranyingi “tunatingwa”, “tunashindwa”, na “majaribu, ugumu na machozi” na “mengi yanayoumiza moyo”. Lakini Bwana anatuambia kupitia neno lake kwamba “Mbingu Itakuwa Bora Kuliko Vyote”.

Dhawabu ya uanafunzi

Kutoka katika kalamu ya Paulo:

Mtu aliyeshinda ugumu mwingi. 2 Kor. 11:23-25, “*Wao ni wahudumu wa Kristo? (nanena kiwazimu), mimi ni zaidi; katika taabu kuzidi sana; katika vifungo kuzidi sana; katika mapigo kupita kiasi; katika mauti mara nyingi. Kwa Wayahudi mara tano nalipata mapigo arobaini kasoro moja,. Mara tatu nalipigwa kwa bakora; mara tatu nalivunjikiwa jahazi; kuchwa kucha nimepata kukaa kilindini;*”

Lakini bado akaangalia mbele katika:

Nyumba isiyojengwa kwa mikono. 2 Kor. 5:1, “*Kwa maana twajua ya kuwa nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jingo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni.*”

Utajiri wa rehema za Mungu. Efe. 2:7, “*Ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu.*”

Mabadiliko ya utukufu. Fil. 3: 20-21, “*Kwa maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni, kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote view chini yake.*”

Taji la haki. 2 Tim. 4:8, “*Baada ya hayo <u>nimewekewa taji ya haki</u>, ambayo Bwana mhukumu mwenye haki, <u>atanipa siku ile</u>; wala si mimi tu, bali na watu wote pia waliopenda kufunuliwa kwake.*”

Ufalme ulio wa kimbingu. 2 Tim. 4:18, “*Bwana atanikoa na kila neno baya, na <u>kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni</u>. Utukufu una yeye <u>milele na milele</u>. Amina.*”

Vilevile mtu aliyevumilia magumu, aliyeandika kuhusu mitu wote:

1 Kor. 4:9-13, “*Maana nadhani ya kuwa Mungu ametutoa sisi mitume mwisho, kama watu waliohukumiwa wauawe kwa sababu tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu. Sisi tu wapumbavu kwa ajili ya Kristo, lakini ninyi ni wenye akili katika Kristo; sisi tu dhaifu, lakini ninyi mna nguvu; ninyi mna utukufu lakini sisi hatupati heshima. Hata saa hii ya sasa, tuna njaa na kiu, tu uchi, twapigwa ngumi, tena hatuna makao; tena twataabika*

tukifanya kazi kwa mikono yetu wenyewe. Tukitukanwa twabariki, tukiudhiwa twastahimili; tukisingiziwa twasihi; tumefanywa kama takataka za dunia, na tama ya vitu vyote hata sasa."

Bado Paulo alitazama mbele katika:

Urithi uliotunzwa mbinguni. Petro aliandika: 1 Pet. 1:4, "*Tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.*"

Mbingu mpya nan chi mpya, ambamo wenye haki wanakaa. 2 Pet. 3:13-14, "*Lakini kama ilivyo ahadi yake mnatazamia mbingu mpya nan chi mpya ambayo haki yakaa ndani yake. Kwa hiyo wapenzi kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amnai kuwa hamna mawaa wala aibu mbele zake.*"

Kutoka katika kalamu ya Yohana:

Mtu aliyekumbana na madhila mengi na utumwa. Ufu. 1:9, "*Mimi Yohana ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.*"

Bado alibarikiwa kuonyeshwa:

Furaha ya wale walioshinda mateso.

- Ufu. 7:9-10, "*Baada ya hayo nikaona na tazama mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa, na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele ya Mwana Kondoo, wamevikwa mavazi meupe, wana matawi ya mitende mikononi mwao; wakilia kwa sauti kuu wakisema, Wokovu una Mungu wetu akatiye katika kiti cha enzi, na Mwana Kondoo.*"
- Ufu. 7:13-17, "*Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je! Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Nikamwambia Bwana wangu, wajua wewe. Akaniambia hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana Kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, nay eye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena , wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana kondoo aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.*"

Makao ya waliokombolewa, milele na Mungu.

- Ufu. 21: 1-7, "*Kisha nikaona mbingu mpya nan chi mpya; kwa maana mbingu za kwanza nan chi ya kwanza zimekwisha kupita wala hapana bahari tena. Name nikauona mji ule mtakatifu Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Nikasikia sauti kubwa*

kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, tazama maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwishaa kupita. Na yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, tazama nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia andika ya kwamba maneno hayo ni amini na kweli. Akanimbia imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima bure. Yeye ashindaye atayaarithi haya, name nitakuwa Mungu wake, naye atakuwa mwanangu."

- Ufu. 21: 10-11, "*Akanichukua katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu Yerusalemu, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu; wenye utukufu wa Mungu, na mwangaza wake ulikuwa mfano wa kito chenye thamani nyingi kama kito cha yaspi, safi kama bilauri;*"
- Ufu. 21: 22-22:5, "*Nami nikaona hekalu ndani yake; kwa maana Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana Kondoo, ndio hekalu lake. Na mji ule hauhitaji jua wala mwezi kuuangaza kwa maana utukufu wa Mungu huutia nuru, na taa yake ni Mwana Kondoo. Na mataifa watatembea katika nuru yake. Na wafalme wan chi huleta utukufu wao ndani yake. Na milango yake haitafungwa kamwe mchana; kwa maana humo hamna usiku. Nao wataleta utukufu na heshi ya mataifa ndaani yake. Na ndani yake hakitaaingia kamwe chochote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu chaa uzima cha Mwana Kondoo. Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele.*"

Hitimisho

Je kuna ulinganifu kati ya miaka michache ya utumishi, hata katika mateso na umilele yenye furaha mbele za Mungu?

"Hakika Mbingu Itakuwa Bora Kuliko Vyote"!

Tumesoma maneno ya wakina Paulo, Petro, na Yohana. Vipi kama wangerudi na kuongea nasi leo? Vipi kama wapendwa wetu waliokufa ndani ya Kristo wangerudi na kuongea nasi leo? Je wasingetuambia "Hakika Mbingu Itakuwa Bora Kuliko vyote"?

Gharama yoyote ya kumfuata Yesu katika maisha haya, maneno ya wimbo huu na ahadi ya maandiko Matakatifu yatukumbushe na kutufariji kuwa waaminifu na kuvumilia.

Heb. 10:35-36, "*Basi msiute ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi.*"